# UCHAGUZI

Jarida la Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Toleo Na. 20 Mei, 2024

HALIUZWI




## Uboreshaji wa Daftari la kudumu la Wapiga Kura kuanza Julai Mosi, 2024

## Uchaguzi Mdogo Jimbo la Kwahani Kufanyika Juni 8, 2024



# Sifa na Kukosa Sifa za Kuandikishwa kuwa Mpiga Kura

Ifahamu Tume

**Kifungu cha 9 (1) na (2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024** kimeeleza kuhusu sifa za mtu anayeweza kuandikishwa kuwa mpiga kura kama ifuatavyo:-

(i) awe raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka kumi na nane na ambaye hajapoteza sifa chini ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote, atastahili kuandikishwa kuwa mpiga kura chini ya masharti ya Sheria hii.

(ii) mtanzania yeyote ambaye hajapoteza sifa chini ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote, ambaye wakati au kabla ya tarehe ya uchaguzi atakuwa ametimiza umri wa miaka kumi na nane.

Aidha, kwa kuzingatia masharti ya **kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024** inaeleza kuwa mtu hatakuwa na sifa ya kuandikishwa au hataandikishwa kuwa mpiga kura ikiwa:-

(i) yuko chini ya kiapo cha utii kwa nchi nyingine tofauti na Tanzania;

(ii) katika sheria yoyote inayotumika Tanzania, imethibitika kuwa hana akili timamu au amewekwa kizuizini kama mhalifu mwenye ugonjwa wa akili au amewekwa kuzuizini kwa ridhaa ya Rais;

(iii) ametiwa hatiani kwa kosa ambalo adhabu yake ni kifo au anatumikia kifungo kwa kosa ambalo adhabu yake inazidi miezi sita iliyotolewa na mahakama au kama ilivyobadilishwa na mamlaka yenye dhamana; au

(iv) amepoteza sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura chini ya masharti ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote inayotumika kuhusu makosa yanayohusiana na uchaguzi wowote.

# Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Kuanza Julai Mwaka huu

**Na Mwandishi Wetu, Zanzibar**

Uzinduzi wa zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura utafanyika tarehe 01 Julai, 2024 mkoani Kigoma na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB).



**Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji (Rufaa) Jacobs Mwambegele akizungumza na waandishi wa habari Mjini Unguja, Zanzibar, tarehe 15 Mei, 2024, ambapo ametangaza kuwa uzinduzi wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura utafanyika tarehe 01 Julai, 202*4.***

Akizungumza na waandishi wa habari Mjini Unguja, Zanzibar, leo tarehe 15 Mei, 2024, Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji (Rufaa) Jacobs Mwambegele amesema kuwa zoezi hilo litakapokamilika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura linatarajiwa kuwa na wapiga kura 34,746,638.

"Kwa kuzingatia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Daftari linatarajiwa kuwa na wapiga kura 34,746,638 kutoka 29,754,699 ya mwaka 2020 hili ni ongezeko la wapiga kura wapya 5,586,433 sawa na asilimia 18.7," amesema Jaji Mwambegele.

Ameongeza kuwa katika zoezi hilo wapiga kura 4,369,531 wanatarajiwa kuboresha taarifa zao na wapiga kura 594,494 wataondolewa katika Daftari kwa kupoteza sifa za kuwa wapiga kura.

Kuhusu idadi ya vituo, Jaji Mwambegele amesema Tume ilifanya uhakiki wa vituo vya kuandikishia wapiga kura mwaka 2023 ambapo baada ya zoezi hilo iliamuliwa kuwa vituo vya kupigia kura vitakavyotumika kwenye uboreshaji wa Daftari ni 40,126.

"Kabla ya uhakiki huo wa vituo, kulikuwa na vituo 37,814 ambavyo vilitumika kuandikisha wapiga kura mwaka 2019/2020. Baada ya zoezi hilo la uhakiki, jumla ya vituo 40,126 vitatumika kwenye zoezi la uboreshaji wa Daftari mwaka 2024 ambapo kati ya vituo hivyo, 39,709 ni vya Tanzania Bara na vituo 417 ni vya Zanzibar," amesema Jaji Mwambegele.

Amefafanua kuwa siku ya uzinduzi ndiyo siku ambayo pia uboreshaji utaanza katika mkoa wa Kigoma na kuendelea katika mikoa mingine ya Katavi, Rukwa na Tabora.

"Kwa lengo la kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi, uboreshaji utafanyika kwenye mizunguko 13 itakayobainishwa kwenye ratiba. Aidha, zoezi hili litaendeshwa kwa siku saba kwenye kila kituo cha kuandikisha wapiga kura," amesema Jaji Mwambegele.

Amesema kuwa zoezi hilo litahusu kuandikisha wapiga kura wapya ambao ni raia wa Tanzania wenye umri wa miaka 18 na zaidi na watakaotimiza umri huo ifikapo tarehe ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 pamoja na wale ambao hawajapoteza sifa kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi au sheria nyingine yeyote.

"Zoezi hilo pia litatoa fursa kwa wapiga kura walioandikishwa awali na ambao wamehama kutoka mkoa au wilaya moja kwenda nyingine waweze kuhamisha taarifa zao kutoka kata au jimbo walioandikishwa awali na kutoa fursa kwa wapiga kura walioandikishwa kurebisha taarifa zao yakiwemo majina….," amesema Jaji Mwambegele.

Mwenyekiti huyo amesema kuwa zoezi hilo la uboreshaji wa Daftari litahusisha pia kutoa kadi mpya kwa wapiga kura waliopoteza au kadi zao kuharibika na kuondoa wapiga kura waliopoteza sifa za kuwemo kwenye Daftari kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuukana uraia wa Tanzania na kifo.

"Kwa upande wa Zanzibar uboreshaji wa Daftari utamhusu mtu yeyote aliyepo Zanzibar ambaye hana sifa za kuandikishwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar lakini ana sifa ya kumchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano," amesema Jaji Mwambegele.

Amesema Tume imefanya ununuzi wa vifaa vya uandikishaji ikiwemo ununuzi wa BVR Kits 6,000 zinazotumia vishikwambi kuchukua taarifa za wapiga kura ikiwemo picha, saini na alama za vidole.

"Tofauti na mashine za BVR zilizotumika katika uboreshaji wa mwaka 2015 na 2020 zilizokuwa na uzito wa kilo 35, BVR Kits za awamu hii ni nyepesi zenye uzito wa kilo 18 ambazo zitaweza kubebeka kwa urahisi," amesema Jaji Mwambegele.

Amesema, Tume imeanzisha mfumo wa uboreshaji kwa njia ya mtandao uitwao Online Voters Registration System (OVRS) ambao utamuwezesha mpiga kura aliyemo kwenye Daftari kuanzisha mchakato wa awali wa kuboresha taarifa zake kwa njia ya mtandao kwa kutumia simu ya mkononi au kompyuta.

"Baada ya kukamilisha mchakato kwa njia ya mtandao mpiga kura atalazimika kufika kituo cha kuandikisha wapiga kura ili kukamilisha mchakato na kupatiwa kadi yake ya mpiga kura," amesema Jaji Mwambegele.

# Tujitokeze kushiriki uchaguzi mdogo Jimbo la Kwahani

## Tahariri

Tarehe 8 Juni 2024, Wapiga Kura wa Jimbo la Kwahani Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar wanatarajiwa kupiga kura kwenye uchaguzi mdogo wa ubunge katika jimbo hilo.

Uchaguzi huu ni fursa adhimu kwa wapiga kura wa Jimbo la Kwahani kumchagua kiongozi wao na hivyo tunawahimiza kushiriki kikamilifu katika uchaguzi huo ili waweze kuitumia haki yao ya kidemokrasia.

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imekwishatangaza kuwa uchaguzi huo utafanyika tarehe 8 Juni, 2024 na fomu za uteuzi kwa ajili ya uchaguzi huo zilitolewa kuanzia tarehe 17 hadi 23 Mei 2024.

Uteuzi wa wagombea umepangwa kufanyika tarehe 23 Mei 2024, na kampeni kwa ajili ya uchaguzi huo zimepangwa kufanyika kuanzia tarehe 24 Mei 2024 hadi tarehe 7 Juni 2024.

Hivyo tunapenda kutumia nafasi hii kuwasihi wapiga kura na wananchi wa Jimbo la Kwahani kuzingatia amani na utulivu katika kipindi hiki cha uchaguzi mdogo wa jimbo hilo.

Pia, tunasisitiza umuhimu wa wagombea kufanya kampeni za amani na kistaarabu.

Tunawasihi wagombea, vyama vya siasa na wafuasi wao kujenga mazingira ya kuheshimiana na kuvumiliana wakati wa kipindi chote cha uchaguzi mdogo.

Aidha ni vyema wagombea, vyama vya siasa na wafuasi wao wakahakikisha kwamba wanayaheshimu maadili ya uchaguzi hususani wakati wa kampeni.

Tunawasihi wananchi wote wa Kwahani kujitokeza kwa wingi siku ya uchaguzi huo ili wamchague kiongozi wanayemtaka.




**Endelea kufuatilia Kurasa za Mitandao ya Kijamii ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na Website ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, ili kupata habari zinazohusu Tume hususani katika kipindi cha Uboreshaji wa Daftari la kudumu la Wapiga Kura.**

# Tume kuwaandikisha Wafungwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura




**Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Bw. Kailima, R. K akifafanua jambo wakati wa mahojiano kwenye kipindi cha Jambo kinachorushwa na TBC1 jijini Dar es Salaam tarehe 17 Mei, 2024. Pamoja naye ni mtangazaji wa kipindi hicho, Janeth Leornard.**

**Na Mwandishi Wetu, Dar es Salaam**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi kwa mara ya kwanza itawaandikisha wafungwa kwa upande wa Tanzania Bara na wanafunzi wa vyuo vya mafunzo kwa upande wa Zanzibar na kuwaruhusu wapiga kura kuanzisha mchakato wa kuboresha taarifa zao kwa njia ya mtandao.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Bw. Kailima R. K tarehe 17 Mei, 2024 wakati akifanya mahojiano maalum kwenye kipindi cha Jambo kinachorushwa hewani na kituo cha televisheni cha TBC1 jijini Dar es Salaam.

Amesema uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura unaotarajiwa kuanza tarehe 1 Julai, 2024 utakuwa na mambo mapya kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwaandikisha wafungwa na wanafunzi wa vyuo vya mafunzo.

Kailima amefafanua kuwa utaratibu wa kuandikisha wafungwa na wanafunzi utazingatia matakwa ya sheria ambapo waliohukumiwa kifungo cha chini ya miezi sita ndio watakaoandikishwa.

Aidha, kwa upande wa Tanzania Bara kuna vituo vya kuandikisha wapiga kura 130 vilivyopo kwenye magereza na kwa upande wa Zanzibar kuna vituo 10 vilivyopo kwenye vyuo vya mafunzo.

Ameongeza kuwa mbali na kuwaandikisha wafungwa na wanafunzi wa vyuo vya mafunzo uboreshaji huo utawaruhusu wapiga kura kuanzisha mchakato wa kuboresha taarifa zao kwa njia ya mtandao.

Bw. Kailima amesema Tume imejenga mfumo ujulikanao kama OVRS (Online Voters Registration System) utakaomwezesha mpiga kura anayeboresha taarifa zake kuanzisha mchakato mtandaoni na baadae kwenda kwenye kituo ili kukamilisha taratibu na kupata kadi yake ya mpiga kura.

"Uboreshaji wa taarifa kwa njia ya mtandao una masharti, kwa wale ambao wanataka kurekebisha taarifa zao ni lazima wawe na namba ya NIDA, lakini, mpiga kura anayehamisha taarifa zake hatalazimika kuwa na namba ya NIDA....," amesema Bw. Kailima.

Amefafanua kuwa namba ya NIDA ni muhimu kwa ajili ya kufanya uhakiki wa taarifa za mpiga kura ambazo zinarekebishwa kwenye Daftari.

Mkurugenzi huyo wa Uchaguzi amefafanua kuwa, wanaokwenda vituoni kujiandikisha kwa mara ya kwanza hawatalazimika kuwa na namba ya NIDA.

# Wagombea 14 wateuliwa kuwania Ubunge Jimbo la Kwahani



**Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Kwahani, Bi. Safia Iddi Muhammad akibandika fomu za uteuzi za wagombea 14 kutoka vyama vya siasa vyenye usajili kamili walioteuliwa kuwania nafasi ya kiti cha Ubunge Jimbo la Kwahani. Uteuzi wa wagombea hao ulifanyika tarehe 23 Mei, 2024.**

Wagombea 14 kutoka vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu wameteuliwa na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) kushiriki katika uchaguzi mdogo wa ubunge katika jimbo la Kwahani, wilaya ya Mjini, mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar.

Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Kwahani, Bi. Safia Iddi Muhammad amesema wagombea tisa kati ya hao waliojitokeza kuchukua fomu na kuzirejesha ndani ya muda uliopangwa ni wanawake na watano ni wanaume.

Fomu za kuwania ubunge katika jimbo hilo zilianza kutolewa kuanzia tarehe 17 hadi 23 Mei, 2024, ambayo pia ilikuwa siku ya uteuzi.

Bi. Safia amesema zoezi la uchukuaji na urejeshaji wa fomu za uteuzi limekwenda vizuri na amevipongeza vyama vyote vilivyojitokeza kugombea nafasi hiyo.

"Zoezi la uteuzi wa wagombea katika Jimbo la Kwahani limekwenda vizuri na tayari majina ya wagombea 14 waliojitokeza kuchukua fomu na kuzirejesha wameteuliwa kuwania kiti hicho," alisema Bi. Safia.

Msimamizi huyo wa Uchaguzi Jimbo la Kwahani amewataja wagombea walioteuliwa na vyama vyao katika mabano kuwa ni Bw. Bashir Yatabu Said (Demokrasia Makaini), Bi. Nuru Abdulla Shamte (DP), Bi. Mwanakombo Hamad Hassan (NLD), Bi. Zainab Maulid Abdallah (CCK), Bi. Tatu Omary Mungi (UPDP), Bw. Khamis Yussuuf Mussa (CCM), na Bi. Jarade Ased Khamis (AAFP).

Wengine ni Bw. Kombo Ali Juma (NRA), Bi. Shara Amran Khamis (ADC), Bi. Naima Salum Hamad (UDP), Bi. Madina Mwalim Hamad (ADA TADEA), Bw. Amour Haji Ali (SAU), Bi. Mashavu Alawi Haji (UMD), na Bw. Abdi Khamis Ramadhan (CUF).

Bi. Safia amesema tayari ameshakutana na wagombea wa vyama vyote na wapo tayari kuanza kampeni.

Kwa mujibu wa taarifa ya INEC iliyotolewa kwa umma na kusainiwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa INEC, Bw. Kailima R. K jijini Dodoma tarehe 02 Mei, 2024, kampeni kwa ajili ya uchaguzi huo zitafanyika kuanzia tarehe 24 Mei, 2024 hadi tarehe 07 Juni, 2024 na uchaguzi utafanyika tarehe 08 Juni, 2024.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

## TANGAZO LA MWALIKO KWA TAASISI NA ASASI ZA KIRAIA ZENYE NIA YA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA WAKATI WA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA MWAKA 2024

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kufanya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Mwaka 2024. Uboreshaji huo utaanza tarehe 01 Julai, 2024 katika Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora. Ratiba ya mikoa mingine itatangazwa kadri Tume itakavyokuwa inaendelea na zoezi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 10(1)(g) na (h) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024, Tume ina wajibu wa kutoa elimu ya mpiga kura nchini, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi za kiraia zinazotoa elimu hiyo.

Hivyo, kupitia tangazo hili, Tume inakaribisha maombi kutoka taasisi na asasi za kiraia nchini zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura 2024 kama ilivyoainishwa kwenye jedwali.

Taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura zinatakiwa kuwasilisha maombi yao katika mfumo wa kusajili watazamaji, asasi za kiraia na vyombo vya habari (Accreditation Management System - AMS) unaopatikana katika anwani ya *https://ams.inec.go.tz*

Maombi hayo yatapokelewa kuanzia tarehe **17 hadi 30 Mei, 2024.**

Taasisi au asasi ya kiraia yenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura inatakiwa kukidhi vigezo vifuatavyo:-

i. iwe imesajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania;

ii. iwe imetuma maombi kupitia mfumo wa Accreditation Management System (AMS) kupitia anwani ya *https://ams.inec.go.tz*

iii. iwe imefanya kazi nchini kwa kipindi kisichopungua miezi sita tangu kusajiliwa kwake;

iv. ikiwa taasisi au asasi ya kiraia inahusisha watendaji wa kimataifa, miongoni mwa watendaji wake wakuu, wawili ambao taarifa zao zitawasilishwa wanapaswa wawe Watanzania;

v. katika utendaji wake, iwe haijahusishwa na uchochezi au kuvuruga amani;

vi. iwe na uzoefu wa kutoa elimu ya mpiga kura; na

vii. iwe tayari kujigharamia katika kutoa elimu ya mpiga kura.

Aidha, taasisi au asasi ya kiraia itakapowasilisha maombi katika mfumo, inatakiwa kutekeleza yafuatayo:-

i. kuambatisha nakala au kivuli cha cheti cha usajili;

ii. kuambatisha nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi husika;

iii. kujaza majina matatu ya viongozi wa juu wa taasisi au asasi husika;

iv. kujaza anwani kamili ya makazi na namba za simu za ofisi na za viongozi wake;

v. kuainisha vyanzo vya fedha zitakazotumika katika utelekelezaji wa jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura;

2

vi. kuambatisha ratiba itakayoonesha tarehe na mahali elimu ya mpiga kura itakapotolewa katika halmashauri husika; na

vii. kuorodhesha katika mfumo watendaji watakaotoa elimu ya mpiga kura walioteuliwa na taasisi au asasi iliyopewa kibali.

**Tume haitahusika na utoaji wa rasilimali fedha au rasilimali nyingine kwa ajili ya kugharamia zoezi la utoaji wa elimu ya mpiga kura kwa taasisi au asasi za kiraia zitakazopewa kibali.**

Limetolewa leo tarehe 17 Mei, 2024 na:

Kailima, R. K
<u>MKURUGENZI WA UCHAGUZI</u>

# "Kujiandikisha kuwa Mpiga Kura ni msingi wa uchaguzi bora"

# Uchaguzi Mdogo Jimbo la Kwahani Kufanyika Juni 8, 2024



**Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Bw. Kailima, R. K akifafanua jambo wakati akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) katika ofisi za Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi zilizopo Njedengwa jijini Dodoma.**

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) imetangaza kuwa uchaguzi mdogo wa Jimbo la Kwahani lililopo Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar utafanyika tarehe 08 Juni, 2024.

Taarifa kwa umma iliyotolewa na kusainiwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa INEC, Bw. Kailima, R. K jijini Dodoma tarehe 02 Mei, 2024 imesema kwamba fomu za uteuzi kwa ajili ya uchaguzi huo mdogo zitatolewa kuanzia tarehe 17 hadi 23 Mei, 2024.

Taarifa hiyo imefafanua kuwa uteuzi wa wagombea utafanyika tarehe 23 Mei, 2024 na kampeni kwa ajili ya uchaguzi huo zitafanyika kuanzia tarehe 24 Mei, 2024 hadi tarehe 07 Juni, 2024.

Tume imetangaza uchaguzi huo mdogo kufuatia taarifa ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iliyomtaarifu Mwenyekiti wa Tume kuhusu uwepo wa nafasi wazi ya ubunge katika Jimbo la Kwahani.

Spika ametoa taarifa hiyo kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 49(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka, 2024.

"Kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 49(1)(b) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, Tume inatoa taarifa kwa umma kuhusu uwepo wa uchaguzi mdogo wa ubunge katika Jimbo la Kwahani lililopo Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar," imesema sehemu ya taarifa hiyo.

Tume imevikumbusha vyama vya siasa, wagombea na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia Katiba, sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi, taratibu, miongozo na maelekezo ya Tume katika kipindi cha uchaguzi huo mdogo.

# Matukio katika Picha




**Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Bw. Kailima, R. K akifafanua jambo wakati wa mahojiano kwenye kipindi cha Jambo kinachorushwa na TBC1 jijini Dar es Salaam tarehe 17 Mei, 2024. Kulia ni mtangazaji wa kipindi hicho, Janeth Leornard na Rajab Rajab.**



**Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji (Rufaa) Jacobs Mwambegele (katikati) akizungumza na waandishi wa habari Mjini Unguja, Zanzibar, tarehe 15 Mei, 2024, ambapo ametangaza kuwa uzinduzi wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura utafanyika tarehe 01 Julai, 2024. Kushoto kwake ni Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume, Bw. Kailima R. K na kulia ni Makamu Mwenyekiti wa Tume, Mhe. Jaji (Rufaa) Mstaafu, Mbarouk Salim Mbarouk.**



Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji (Rufaa) Jacobs Mwambegele akizungumza na waandishi wa habari Mjini Unguja, Zanzibar, tarehe 15 Mei, 2024, ambapo ametangaza kuwa uzinduzi wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura utafanyika tarehe 01 Julai, 2024



Baadhi ya wanachama na wagombea wa Vyama mbalimbali vya siasa vilivyosimamisha wagombea katika Uchaguzi Mdogo wa Jimbo la Kwahani Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar wakikagua fomu za uteuzi za wagombea zilizobandikwa baada ya uteuzi mnamo tarehe 23 Mei, 2024.





**Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi**
**Makao Makuu Dodoma,**
**5 Barabara ya Uchaguzi,**
**41107 Njedengwa,**
**Uchaguzi House,**
**Anuani: S.L.P 358, Dodoma**
**Namba ya simu: +255 26 2962345-8**
**Nukushi: +255 26 2962348**
**Barua pepe: Uchaguzi@inec.go.tz**

www.inec.go.tz
tumeyauchaguzi_tanzania
Tume ya Uchaguzi-TZ
Tume ya Uchaguzi-tz
INEC-TZ Online TV